

OFISI YA RAISI – TAMISEMI

HALIMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO,
S.L.P 324,
KYELA.

SIMU – 0766769770

KUMB. NA. KFS/.....

NDG. MZAZI/ MLEZI WA-----

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO

1. UTANGULIZI

Tunayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari kafundo kuanza kidato cha kwanza mwaka 2021.

Muhula wa kwanza wa masomo, utaanza tarehe. Inatakiwa kuripoti shuleni tarehe mwisho wa kuripoti ni tarehe .

2. MAHITAJI YA SHULE

Mwanafunzi arfikapo shuleni anatakiwa afike na vitu vifuatavyo.

2.1: SARE ZA SHULE WAVULANA

- Suluali mbili, zisiswe “**MODO WALA SIMPLE JINSI**” zikiwa hivo utarudishwa ili ushone sare ya shule.

RANGI – Moja iwe kijani kibichi na

_Nyingine iwe Zambarau nyeusi

- Mashati mawili meupe ya tetroni yenye mikono mifupi na yasiwe mafupi.
- Viatu vyeusi vyenye kamba jozi mbili

- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Sweta ya biue moja.
- T-shirt rangi ya bluu yenye kola nyeupe. Pia inaweza kupatikana shuleni kwa Tshs. 10,000/=

2.2: SARE ZA SHULE WASICHANA

- Shati nyeupe mbili(tetroni) za mikono mifupi zisibane wala zisiwe fupi.
- Sketi mbili, moja ya marinda ya kawaida rangi ya kijani kibichi, na nyingine ya rinda box rangi ya zambarau nyeusi zoteziwe ndefu ziguse viatu. Zisipogusa viatu utarudishwa.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba jozi mbili.
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Hijabu rangi nyeupe kwa watakaotumia
- Sweta rangi ya bluu
- T-shirt rangi ya bluu yenye kola nyeupe. Pia inaweza kupatikana shuleni kwa Tshs. 10,000/=

3. VIFAA VYA MICHEZO

- Track suti rangi ya bluu kwa ajili ya michezo
- Raba jozi moja na Soksi ndefu jozi moja vitakaguliwa shuleni siku ya kuripoti

4. VIFAA VYA MASOMO – TAALUMA.

- Unatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo kwa ajili ya masomo,
- ❖ Madaftari kumi (10) kaunta buku quire 3 na quire 4 kati ya hayo.
- ❖ Kaunta buku moja quire 4 litakabidhiwa ofisi ya taaluma.
- ❖ Daftari ndogo za (sh.300/=) ziwe tisa kwa ajili ya majaribio na mazoezi.
- ❖ Kalamu za wino rangi ya blue, kalamu za risasi(penseli), rula na mkebe wa hesabu
- ❖ Dictionary ya kiingeleza kwa kiingeleza ya mwanafunzi(student dictionary)
- ❖ Begi zuri la kubebea daftari na vifaa vingine.Sio Rambo wala foronya.

5. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha ,inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi Elimu ya juu, Teknolojia na mafunzo ya Ufundi yenye

dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Raisi TAMISEMI, Utumishi na utawala bora wenye majukumu ya usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumula ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule, ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(Preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba za shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za Umma.

5.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- a) Wizi
- b) Uasherati na Ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile Bangi, Pombe, Cocaine, Mirungi, Kuberi, Madrax, Heroine n.k
- e) Kupigana na kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya taifa
- h) Kuwa mjamzito au Kupata mimba
- i) Kuoza au Kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na Usalama wa shule au watu.
- l) Kuwa na simu ya mkononi

6.TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA
KUYATEKELEZA KIKAMILIFU

GREGORY R.
MKUU WA SHULE